# DKT HARRISON MWAKYEMBE AKABIDHIWA RIPOTI YA UHAKIKI WA ASASI ZA KIRAIA



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe Dkt Harrison Mwakyembe amekabidhiwa Ripoti ya uhakiki ya pamoja kutoka kwa Taasisi za Serikali zinazofanya kazi ya usajili wa Asasi za kiraia pamoja na utekelezaji wa agizo la kusitisha asasi zote zitakazobainika kukiuka sheria na taratibu za usajili, tukio hilo la makabidhiano limefanyika hii leo katika ukumbi wa Mikutano wa RITA Jijini Dar es salaam.

Kwa upande wa RITA Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Bi. Emmy Hudson amesema kuwa Wakala ulichukua hatua mbalimbali ikiwemo kusitisha kwa muda wa usajili wa Bodi za wadhamini ,kutoa tangazo la kuwataka wadhamini kuhuisha taarifa zao pamoja na kuingiza taarifa kwenye mfumo wa kielectroniki(kanzi data ya RITA) sambamba na kutembelea Bodi za wadhamini katika Wilaya mbalimbali.

Matokeo ya utekelezaji wa zoezi hilo kwa RITA lililodumu kwa miezi mitatu na kusema kuwa jumla ya bodi za wadhamini 1944 kati ya 5262 zilizosajiliwa ziliwasilisha taarifa zao kwa njia mbalimbali ikiwemo barua pepe na wengine kufika ofisini.
Jumla ya Taasisi 180 zimekwisha pelekwa kwenye gazeti la Serikali kwa ajili ya kuchapishwa ili kuzitangaza kufutwa rasmi kwa mujibu wa sheria ambapo mwisho wa mwezi Agosti mwaka huu taasisi zilizofutwa zitatangazwa kwenye vyombo vya habari.

Hata hivyo zoezi hilo litakuwa endelevu kwa Wakala kutembelea na kukagua Taasisi zilizosajiliwa na kuendelea kutoa Elimu ya Udhamini kwa wananchi na kuhamasisha Taasisi zinazomiliki mali bila kusajili Bodi za Wadhamini kujitokeza ili ziweze kusajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Naye kaimu Msajili wa Asasi za Kidini na Kiraia kutoka Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi Bi Marline Komba amesema kwa kipindi cha mwaka 2016 wamefanikiwa kuchambua Asasi za Kiraia zipatazo 3000 na kubaini dosari mbalimbali zikiwemo kutohuishwa taarifa na kubainisha majukumu yao na hivyo Wizara kuamua itafuta orodha hiyo katika daftari la Msajili na kubakia na Asasi 11500 ambapo uhakiki bado unaendelea na zitakazobainika zitawekwa katika orodha ya kuzifuta.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Bw Baraka Leonard amesema Wizara yao imesajili zaidi ya Mashirika 2000 ingawaje taarifa zinaonesha yapo Mashirika yanayojiita NGO'S ambayo yanafanya kazi bila ya kusajiliwa na hivyo vitachukuliwa hatua za kisheria.
Ripoti ya uchambuzi na uhakiki iliyowasilishwa imebaini kuwepo kwa mingiliano ya taratibu za usajili kupitia Taasisi moja hadi nyingine kutokana na masharti ya kisheria ,hatua za usajili kutokamilishwa katika Taasisi moja kunakotokana na matakwa ya kisheria kwa maana ya usajili katika baadhi ya asasi ili uweze kukamilika ni lazima kupitia katika Taasisi zaidi ya moja, vilevile kukosekana kwa mfumo wa kisheria unaozitaka Taasisi zinazofanya usajili kubadilishana taarifa na Taasisi nyingine za Serikali kuhusu masuala ya usajili na vilevile Taasisi zinazofanya usajili zipo Jijini Dar es salaam pekee na hivyo kuwa mbali na Asasi za kiraia kunakopelekea kushindwa kwa usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Asasi hizo.

Zoezi la uhakiki na ukaguzi wa Bodi ya Wadhamini za Asasi/Taasisi za kiraia lilianza mwezi Machi mwaka huu agizo aliolitoa Mhe Waziri wa Katiba na sharia DKT Harrison Mwakyembe na kutaka kutekelezwa ndani ya miezi mitatu kwa lengo la kubaini Asasi za Kiraia zinazowajibika na zile hewa ili kuchukuliwa hatua za kisheria, baadhi ya Taasisi hizo zilizoagizwa kufanya uhakiki ni RITA, BRELA, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto na Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi .



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe Harrison Mwakyembe akikabidhiwa taarifa ya pamoja ya Taasisi za Serikali zinazojishughulisha na masuala ya usajili wa Asasi za kiraia kutoka kwa naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Bw Amon Mpanju wakati wa mkutano na Waandishi wa habari Hii leo katika ukumbi wa Mikutano wa RITA Jijini Dar es salaam.



Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa agizo la kuhakiki Miunganisho ya Wadhamini katika asasi za kiraia, katikati ni Waziri wa Katiba na Sheria Mhe Harrison Mwakyembe anayefuata kulia kwake ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo Bw Amon Mpanju.




kaimu Msajili wa Asasi za Kidini na Kiraia kutoka Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi Bi Marline Komba akiwasilisha muktasari wa ripoti ya Wizara yake.




Mkurugenzi Msaidizi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, jinsia Wazee na Watoto Bw Baraka Leonard akiwasilisha ripoti ya Wizara yake.



Waandishi wa Habari kutoka vyombo mbalimbali wakifuatilia utangulizi wa ripoti iliyowasilihwa na Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Ufuatiliaji wa Haki Bw Patience Ntwina.



Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Ufuatiliaji Haki Bw Patience Ntwina wa kwanza kulia akiwasilisha kwa ufupi maeneo yaliyobainika kuwa ni kikwazo katika usajili wa Asasi za Kiraia, wakatikati ni Waziri wa Katiba na Sheria Mhe Harrison Mwakyembe na kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo Bw Amon Mpanju.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe Harrison Mwakyembe akitoa ufafanuzi kwa Waandishi wa habari katika mkutano wa kupokea ripoti kutoka kwa Taasisi za Serikali zinazofanya usajili wa Asasi za kiraia hii leo Jijini Dar es salaam, Kulia kwake ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo Bw Amon Mpanju na kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Ufuatiliaji Haki Bw Patience Ntwina.